*Mulika, Na. 42 (2), 217-237*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Tathmini ya Anthropomofiki katika Riwaya ya Shamba la Wanyama

*Waithiru Kago Antony*[1]
Chuo Kikuu cha Laikipia
na
*Sheila Wandera-Simwa*[2]
Chuo Kikuu cha Laikipia
na
*Onyango Ogola James*[3]
Chuo Kikuu cha Laikipia
DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t2.5

**Ikisiri**

Makala haya yanatathmini namna anthropomofiki ilivyotumika katika riwaya ya Shamba la Wanyama ya George Orwell. Orwell ni miongoni mwa waandishi maarufu na waliosifika katika fani na utunzi wa kazi za fasihi zinazokashifu mfumo wa utawala wa kibepari, kwa kutumia mbinu ya anthropomofiki. Lengo kuu la makala haya ni kujadili jinsi ambavyo anthropomofiki imetumiwa na mwandishi katika kukabiliana na ubepari ulimwenguni. Hivyo, makala haya yanajikita katika kujadili mapinduzi yaliyozalishwa na elimu na yaliyowasilishwa kianthropomofiki na George Orwell. Katika kufanikisha tathmini hii, makala haya yaliongozwa na baadhi ya mihimili mikuu ya nadharia ya Uhakikimazingira kama ilivyoasisiwa na Glotfelty, Fromm pamoja na Buell. Mihimili miwili mikuu iliyoongoza tathmini ya makala haya ni uwezo na kifo, na uongozi mbaya na ukoloni mamboleo. Nadharia hii imejikita katika uhakiki wa matini za kifasihi kwa kudhihirisha uhusiano na utegemeano baina ya binadamu na mazingira. Data ya makala haya ilipatikana maktabani. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mwandishi amefanikiwa kukemea ubepari kupitia mbinu ya anthropomofiki katika riwaya teule. Riwaya hii iliteuliwa kwa kudhamiria kutokana na kuwepo kwa suala la mazingira ya binadamu kupitia mbinu ya anthropomofiki.

## 1.0 Utangulizi

Orwell aliiandika riwaya ya *Shamba la Wanyama* mnamo mwaka 1945 katika lugha ya Kiingereza. Hatimaye, ilitolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa mara ya kwanza mwaka 1967 baada ya kutafsiriwa na Fortunatus Kawegere. Riwaya hii inafafanua namna wanayama wanavyoishi katika shamba la Ibura chini ya utawala wa binadamu na baada ya kumuondoa binadamu. Hapo kabla, shamba la wanyama

[1] Baruapepe: kagoantony3@gmail.com
[2] Baruapepe: sheiwande@gmail.com
[3] Baruapepe: a9904279@yahoo.com

lilikuwa linaitwa Shamba la Ibura, ambapo wanyama walitawaliwa na Bwana Mtiki. Hali shambani ilikuwa ya dhuluma na utawala ulikuwa wa kidikteta. Bwana Mtiki alitumia ujeuri na ulaghai kushikilia mamlaka na hakujali hali mbaya ya wanyama. Wanyama waliwafukuza binadamu kutokana na dhuluma na utawala mbaya. Baada ya mapinduzi, Bwana Mtiki na wafanyakazi wake walifukuzwa na wanyama. Shamba la wanyama, baada ya kufukuzwa kwa Bwana Mtiki na wafanyakazi wake, sasa linaongozwa na wanyama wenyewe ambao ni Mkimwa (nguruwe), Mzushi (nguruwe) na Mcheshi (nguruwe). Mkimwa, Mzushi na Mcheshi wanadhibiti mafunzo ya mapinduzi yaliyoasisiwa na marehemu Peusi Mzee na kuyaita “Unyama”. Ingawa, baada ya mapinduzi, wanyama wanashirikiana kwa kila jambo, nguruwe wanadhihirisha ubinafsi-uchoyo. Miezi kumi baadaye, baada ya kufukuzwa, Bw. Mtiki, watu wake pamoja na wasaidizi wengine wanashambulia shamba la wanyama lakini shambulizi lao halifui dafu. Mkimwa anapanga njama za kumwangamiza Mzushi lakini njama hizo zinagonga mwamba. Kwa ujumla, nguruwe wakiongozwa na Mkimwa wanaendeleza uongozi, udhalimu na mauaji kuliko hata binadamu pale shambani. Hili linawahuzunisha sana wanyama. Mkimwa anashirikiana na binadamu katika biashara, majadiliano na ulevi kinyume na sheria za wanyama ambazo zinanajisiwa na Mcheshi mara kwa mara.

George Orwell alitunga kazi hii katika kipindi ambacho kilishuhudia misukosuko na migogoro mingi ulimwenguni kote. Vita vya Pili vya Dunia, mfululizo wa mapinduzi na vita vya wenyewe kwa wenyewe pamoja na vile vya baridi vilishamiri. Kazi hii ilitungwa kwa kuzingatia mbinu ya anthropomofiki. Utunzi wa kisanaa unaotumia mbinu ya anthropomofiki umekuwa nyenzo muhimu sana katika kuusawiri, kuutashtiti na kuurekebisha mfumo wa kikoloni, hasa wa ukoloni mamboleo na mifumo mingine yote ambayo hukiuka haki na kaida za jamii fulani. Madhali George Orwell ni miongoni mwa wasanii wa kazi za fasihi walioanza kuandika kazi zao katika kipindi cha ukoloni mkongwe na hasa ubepari, mtafiti aliamua kuangaza namna ambavyo mtunzi huyu ametumia anthropomofiki kama mbinu mojawapo ya kiutunzi yenye kusudi la kusawiri hali halisi katika jamii, hasa katika kipindi cha ubeperi kama mbinu kwepi na fiche. Orwell ameibua ubinafsi na uchoyo, uharibifu pamoja na uchafuzi wa mazingira ya binadamu kupitia wanyama. Suala la uchafuzi na uharibifu wa mazingira ameliwasilisha kupitia mbinu ya anthropomofiki katika kudhihirisha ‘ubinadamu’ katika ‘unyama’ wa wanyama (Nayar, 2010; Slovic na wengine, 2020; Filipova, 2023; Garrard, 2023).

Katika fasihi, anthropomofiki ni mbinu mojawapo muhimu sana ambayo hutumiwa na wasanii kufanikisha ujumbe wao lengwa kwa hadhira nuiwa kwa ufanisi mkubwa. Mbinu katika fasihi ni njia ambayo mwanafasihi au msanii huchagua kuitumia kuwasilisha maudhui ya kazi yake (Leech, 2013; na Mulokozi, 2017). Mbinu huhusisha uchaguzi wa kutumia vifaa kama vile maneno maalum, muundo maalum wa sentensi, picha, sauti, na mtindo wa kipekee (Onyango, 2011). Kwa

kutumia mbinu mwafaka, mwandishi huweza kuzalisha kazi ya kipekee ya fasihi yenye dhana, mawazo na hadithi za kipekee zinazobeba ujumbe muhimu na mzito kwa hadhira lengwa (Alia, 2017; na Tan, 2019). Hivyo, anthropomofiki ni mbinu ambayo hudhihirika katika kazi za kifasihi na zile za kisayansi hasa za saikolojia mtawalia. Katika utafiti uliozaa makala haya, watafiti waliangaza anthropomofiki kama mbinu ya fasihi, ambayo hutawala katika kazi za maandishi, za picha, za video, mazungumzo na za michoro ya vibonzo mtawalia bila kuvuka kwenye taaluma ya sayansi na elimuviumbe. Hii ni kusema kuwa, makala yanaangazia anthropomofiki kwa misingi ya namna ya uwasilishaji wa suala la mapinduzi yanayozalishwa na elimu. Mafanikio yake yalibainishwa kupitia wanyama wafugwao katika riwaya ya *Shamba la Wanyama* (1945).

## 2.0 Dhana ya Anthropomofiki

Anthropomofiki ni tabia au matokeo ya sifa, hisia na hulka za binadamu kufanywa na kutekelezwa na wanyama, vifaa, viumbe visivyo hai, na/ au hata mimea. Kwa kawaida, binadamu huhusisha sifa, maumbile na hulka za anthropomofiki na wanyama, sanaa, na shani asilia (Megan na wenzake, 2015; Airent, 2018). Kwa mujibu wa Megan na wenzake (2015) pamoja na Airent (2018), anthropomofiki haijajikita katika mifumo maalumu ya imani ila imejikita katika mahusiano na maingiliano. Hivyo, wanasisitiza kuwa, anthropomofiki ni mwelekeo msingi katika binadamu ambao huanza kwenye ukembe na huendelea kushamiri katika maisha yote ya binadamu. Tofauti za anthropomofiki baina ya watoto na watu wazima sio za kiujarabati ila zinazojikita katika uchangamano. Hii ni kwa sababu anthropomofiki katika watoto huwa asilia zaidi kuliko katika watu wazima (Dacey, 2017).

Airent (2018) akiwanukuu Larsen, Lee na Ganea (2018), anasisitiza kuwa anthropomofiki ni maalumu zaidi kwa sifa na hulka za mtindo wa mawazo ya binadamu au athari kwa viumbe visivyo hai. Ingawa anaongeza kuwa hulka hizi za maisha ya binadamu zinapodhihirika katika viumbe visivyo hai, mara nyingi hupitisha pia athari za kimawazo na hali za kihisia. Utafiti huu ulijikita katika mwelekeo wa hulka na sifa bila kuangaza suala la kisaikolojia. Hii ni kwa sababu utafiti wenyewe ni wa kifasihi ambao uliongozwa na nguzo mbili za Nadharia ya Uhakikimazingira. Larsen na wenzake (2018) wanadokeza kuwa anthropomofiki huwa sehemu muhimu na asilia katika maisha ya binadamu. Mathalani, wanaeleza kuwa binadamu huweza kutambua sifa za kuonekana za viumbehai katika vifaa asilia. Kwa mfano, binadamu huweza kuona sura ya binadamu kwenye mwezi kwa kutazama mwali wa mwanga wa mwezi, au farasi katika mawingu wakati wa mchana. Uwezo huu wa kusawiri na kubuni miundo ya viumbe au vifaa tofautitofauti huonekana kuwa wa msingi sana kwa binadamu. Morris, Lesley na Knights (2012) wanaeleza kuwa anthropomofiki huwa asilia na huchipuliwa sanasana na wanyama vipenzi, ambao binadamu huweza kugawana nao muda na hisia za maisha yake. Hivyo basi, katika fasihi, anthropomofiki hutumiwa

kuwasilisha ujumbe mzito, wenye uwezo wa kuzua uhasama, chuki au hata unyanyapaa, kwa njia ya kukwepa lawama wala tuhuma zozote dhidi ya msanii wa kazi fulani ya fasihi (Megan na wenzake, 2015; Airent, 2018).

## 3.0 Msingi wa Nadharia

Makala yameongozwa na Nadharia ya Uhakikimazingira. Nadharia hii iliasisiwa na Glotfelty (1996) pamoja na Buell (1996). Waasisi hawa wanakubaliana kuwa utamaduni wa binadamu huwa na uhusiano na mwingiliano wa moja kwa moja na maumbile. Bladow na Ladino (2018) na Waithiru (2022b) wakiwaunga mkono wanaeleza kuwa, uchanganuzi wa kiuhakikimazingira huhakiki namna ambavyo binadamu, utamaduni, maumbile, utandawazi na ekolojia kwa ujumla, huingiliana na kuathiriana. Kazi ya Orwell imefanikiwa kufafanua masuala yanayoathiri jamii na mazingira yake katika maisha ya mwanandamu. Hivyo, mazingira halisi, ya kisiasa na kiuchumi yameangaziwa katika misingi ya kiuhakikimazingira. Mihimili miwili iliongoza uchanganuzi wa makala haya. Mihimili hiyo ni uwezo na kifo, na uongozi mbaya na ukoloni mamboleo. Mhimili wa uwezo na kifo hufafanua kuwa kutokana na uwezo wa binadamu, hususani wa kutoka mataifa tajiri huweza kusababisha maafa ya viumbe hai na mazingira kwa ujumla. Mathalani, mataifa tajiri huchangia sana uchafuzi wa hewa. Suala hili husababisha ongezeko la joto ulimwenguni na mabadiliko ya tabianchi. Hatimaye, ongezeko la joto na mabadiliko ya tabianchi husababisha kiangazi au mafuriko ambapo viumbe huangamia. Uongozi mbaya na ukoloni mamboleo husababisha ukosefu wa sera, sheria na mikakati madhubuti ya kulinda na kusimamia rasilimali asilia (Waithiru, 2022a). Isitoshe, ukoloni mamboleo husababisha unyonyaji wa rasilimali za Afrika na nchi tajiri pamoja na mashirika ya kigeni, ambayo hayalipi kodi stahiki, hayazingatii viwango vya ubora na usalama, na hayayasikitikii wala kuyawajibikia mazingira (Filipova, 2023). Garrard (2007) anafafanua kuwa masuala ya kiekolojia yanaweza kuwasilishwa kwa jamii kupitia mbinu mbalimbali za sanaa, madhali sanaa, hasa ya fasihi, huingiliana sana na utamaduni wa jamii. Hivyo basi, makala yaliangaza mbinu ya anthropomofiki katika kupitisha ujumbe kwa jamii katika riwaya inayobeza ubepari na kukumbatia usoshalisti, ya *Shamba la Wanyama*.

## 4.0 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Kipengele hiki kinawasilisha mjadala wa matokeo ya utafiti wa makala haya. Mjadala huu uliongozwa na mihimili miwili ya Nadharia ya Uhakikimazingira mintarafu ya lengo kuu la makala. Maeneo kadhaa yamebainishwa kudhihirisha ujitokezaji wa anthropomofiki katika riwaya ya *Shamba La Wanyama*. Maeneo hayo ni uhamasishaji wa mapinduzi, utamaduni na mabadiliko, mapinduzi, elimu, ubepari na uongozi mbaya.

### 4.1 Uhamasishaji wa Mapinduzi

Orwell, kwa kutumia anthropomofiki, anadhihirisha uhamasishaji wa mapinduzi kupitia wanyama katika shamba la Ibura. Orwell kupitia anthropomofiki

anamsawiri mhusika Mbalamwezi (nguruwe dume) kama asili ya mapinduzi katika jamii au taifa. Katika riwaya hiyo, Mbalamwezi anaongoza mapinduzi katika shamba la Ibura la Bwana Mtiki. Hii ni kwa sababu shamba la Ibura linaashiria mataifa fukara ya ulimwenguni ilhali wanyama wanaashiria wananchi ambao hupambana na uongozi mbaya, ulofa, maradhi, maafa, vita vya kikabila, baa la njaa, kwa kubainisha kwa uchache. Wananchi katika mataifa haya huishi maisha ya dhuluma na dhiki chungu nzima. Hali hii inafungamana na mhimili wa uongozi mbaya na ukoloni mamboleo wa Nadharia ya Uhakikimazingira ambapo kutokana na kutowajibika kwa binadamu katika mazingira yake, hukosa kuwekeza katika teknolojia ya miundombinu ya kijani, ambayo huweza kuboresha ufanisi wa nishati; kukuza nishati mbadala na kupunguza uharibifu wa mazingira. Vilevile, kwa misingi hii, Mbalamwezi anawaambia wanyama wenzake kuwa maisha yao ni ya taabu, yenye kuchosha bure na mafupi mno. Anafafanua kuwa wanyama wazaliwapo hupewa kiasi kidogo cha chakula na tena chapwa. Lengo la Mbalamwezi ni kuwahamasisha wanyama dhidi ya maonevu ya binadamu.

Anawakumbusha kuwa baada ya kufanyishwa kazi za sulubu huchinjwa kwa ukatili mkubwa. Anawasisitizia kuwa katika ulimwengu wao hamna mnyama mwenye uhuru, madhali wao huishi maisha ya dhiki na utumwa. Mbalamwezi anaisawiri hali halisi katika mataifa mengi ulimwenguni, hususani Barani Afrika. Hakika, mataifa ya Afrika yana uwezo wa kutosheleza mahitaji na chakula kwa watu wote. Ingawa Afrika ni bara fukara kwa kiwango kikubwa, lina uwezo wa kuleta maisha bora kwa wote waishio juu yake. Mhusika Mbalamwezi anadhihirisha hili kianthropomofiki anaposema, “Udongo wa nchi yetu ni wenye rutuba. Hali yake ni nzuri. Waweza kutoa chakula kingi kwa wanyama wengi zaidi yetu” (uk. 10). Mtunzi Orwell kupitia Mbalamwezi, mhusika katika *Shamba la Wanyama*, anaashiria binadamu kama taashira ya beberu. Mbalamwezi anaeleza kuwa mazao na nguvu zao zote huibwa na binadamu. Anasisitiza kuwa matatizo, changamoto, mateso, dhuluma na mengine yote yanayowakumba wanyama pale shambani Ibura yanaweza kufupishwa kwa neno moja tu, binadamu! Kwa mujibu wa mhimili wa uongozi mbaya na ukoloni mamboleo, binadamu anaashiriwa kama beberu ambaye kupitia ujangili wa ukoloni mamboleo anaendelea kuyanyonya mataifa fukara ya Afrika kiuchumi, kisiasa na kijamii. Binadamu, kama beberu, hutumia bila kutoa.

Mathalani, Mbalamwezi anafafanua kuwa binadamu huwa hatagi mayai, hana maziwa kama ya ng’ombe na hawezi kulivuta jembe likokotwalo kutokana na udhaifu wake. Aidha, hawezi kumkimbiza sungura hadi akamkamata lakini ndiye mtawala na kiongozi mkuu wa wanyama wote. Hili linawahamasisha wanyama kufanya mapinduzi ili kuudidimiza uwezo wa binadamu dhidi yao. Hali hii inafungamana na mhimili wa uwezo na kifo ambapo binadamu mwenye mamlaka huyanajisi mazingira na madhara yake husababisha maangamizi kwa wanyonge, wanyama na mimea kwa ujumla. Inadhihirika kuwa beberu ni dhaifu na huwa analikamua Bara la Afrika rasilimali asilia, huduma za wataalamu, wafanyakazi,

wanariadha na vitu aina aina vya thamani kubwa bila kuchangia chochote wala kwa vyovyote. Aidha, beberu huendeleza utawala dhalimu wa manyanyaso na maonevu, hali inayofungamana na mhimili wa utawala mbaya na ukoloni mamboleo. Kupitia anthropomofiki, Mbalamwezi anawakumbusha wanyama wenzake kuwa, nguvu zao hutifua udongo huku samadi yao ikiutia rutuba ilhali wanachomiliki cha maana ni ngozi ya kila mmoja pekee bila kitu kingine chochote. Hili linaashiria ulofa baina ya wananchi wanaosawiriwa na wanyama.

Kadhalika, Mbalamwezi anawakumbusha ng’ombe kuwa maziwa wanayotoa yanamiminwa tumboni mwa binadamu badala ya kuwakuza ndama wanono. Hili linaashiria jinsi ambavyo beberu hujinufasha mwenyewe kwa kulinyonya Bara la Afrika na kuliacha likidhoofika. Kwa upande mwingine, kuku wanakumbushwa kuhusu mayai waliyoyataga yaliyouzwa sokoni ili kumfaidi binadamu. Mbio naye anakumbushwa kuhusu watoto wake wanne waliouzwa wakiwa na umri wa mwaka mmoja badala ya kumfaa yeye uzeeni. Hili linaashiria biashara ya kuuzwa kwa vijana wenye nguvu kama watumwa kutoka Afrika hadi Ughaibuni. Mbalamwezi anaendelea kuwakumbusha nguruwe walionona kuwa hakuna mnyama hata mmoja aepukanaye na kisu kikali mwishoni. Mathalani, anawaeleza, “Ninyi nguruwe wanono mnaoketi mbele yangu, baada ya mwaka, kila mmoja atalaza kichwa chake penye gogo – tayari kuchinjwa” (uk. 11). Uhamasishaji huu unafanikishwa kupitia mbinu ya anthropomofiki.

Aidha, mbwa nao wanakumbushwa kuwa punde tu meno yao yatakapotoka kutokana na uzee, binadamu atawafungia matofali shingoni na kuwatumbukiza ndani ya dimbwi litakalokuwa karibu. Kwa kutumia mhusika Mbalamwezi, mtunzi Orwell anawahamasisha Waafrika dhidi ya mabeberu wa kisasa. Mwandishi huyu amefanikiwa kukaripia utawala dhalimu wa ukoloni mkongwe. Hali ya kuwaangamiza mbwa wakongwe inawiana na maangamizi ya mazingira ya mataifa duni baada ya kunyofolewa rasilimali asilia na kutumiwa kama shimo la taka na viongozi wa mataifa tajiri. Binadamu anaashiria mkoloni mkongwe aliyewahi kuyatawala mataifa mengi Barani Afrika. Katika kipindi cha sasa, riwaya hii inawahamasisha Waafrika dhidi ya mabeberu wa kisasa. Ingawa mkoloni aliondoka na kumwacha Mwafrika ajitawale, bado baadhi ya watawala huonekana kuwa ni vibaraka wa wakoloni (Waithiru na wenzake, 2021; Waithiru, 2022c). Hii ndiyo sababu Mbalamwezi anawakumbusha wanyama wote kuwa adui yao mkubwa na anayewasababishia ubaya wa maisha ni binadamu na udhalimu wake.

**4.2 Utamaduni na Mabadiliko**

Kupitia ndoto ya Mbalamwezi, Orwell anadhihirisha mchango wa utamaduni katika kuzalisha mabadiliko katika jamii, hasa mabadiliko dhidi ya utawala dhalimu. Mathalani, kupitia ndoto hiyo, mwandishi anadhihirisha kuwa utamaduni una mwingiliano na ugiligili wa moja kwa moja na mabadiliko. Mbalamwezi anawakumbusha wanyama wote kuhusu wimbo uliokuwa ukiimbwa na mamake

kwa ushirikiano na jamaa wengine. Ingawa ni wimbo wa jadi katika utamaduni wa jamii ya nguruwe, Mbalamwezi anaukumbuka na kuwaimbia kwa sauti yake iliyokauka. Wimbo wenyewe unaitwa *Ndugu Zangu e Wanyama,* kuashiria umoja na ushirikiano.

Hivyo, wimbo unaashiria ala nzuri ya kiutamaduni ya kuzalisha mabadiliko dhidi ya utawala dhalimu. Ingawa ujumbe unapaswa kuwa wa kitaashira, upitishaji wa ujumbe umefanikishwa na matumizi ya mbinu ya anthropomofiki. Siku ya furaha ya wanyama inasawiri siku ya kupata uhuru wa nchi fulani Barani Afrika kutoka kwenye pingu za ukoloni mkongwe. Mbalamwezi anawarai wanyama wenzake wapiganie uhuru wao ili hatimaye waibuke washindi dhidi ya mkoloni. Kwa mfano, anaimba:

> Sisi sote tunapaswa,
> Kujitahidi sana,
> Farasi, ng’ombe na mbwa,
> Uhuru kuutafuta (uk. 15).

Wimbo huu uliwapa wanyama ari mpya ya kutaka uhuru. Wanyama kama vile nguruwe na mbwa walichukua muda mfupi kuuelewa wimbo kisha wakauvurumisha ulivyostahili kwa heshima na taadhima ya wimbo mgeni. Baada ya majaribio kadhaa, kwa sauti moja, ng’ombe, farasi, mbwa, kondoo na bata walilialia na shamba lote likapasuka na kuuimba mara tano mfululizo. Tofauti zinazodhihirka baina ya wanyama zinasawiri tofauti zilizopo baina ya watu hususan katika kumaizi na kufasili mambo. Ingawa wanakatishwa ghafla na Bwana Mtiki aliyedhani kuwa Mbweha alikuwa ameingia uani, hawakukata tamaa wala kusita katika mipango yao ya kupigania uhuru wao. Vita vya uhuru wao ni vita vya uhuru wa taifa lao.

**4.3 Mapinduzi**

Mapinduzi yanayozalishwa katika Shamba la Ibura la Bwana Mtiki ni zao la uvivu wa wafanyakazi, na uvivu na ulevi wa Bwana Mtiki. Bwana Mtiki baada ya kupoteza fedha kwa kushindwa mashtaka mahakamani, alibadili mwenendo na kushiriki mno ulevi. Aliupoteza muda mrefu akiketi kivivu kitini huku akivinjari magazeti, mvinyo na kumlisha Jura mabaki ya mkate yaliyochanganywa kwa vileo. Jambo hili lilisababisha bidii ya Bwana Mtiki kufifia na sehemu tofauti za shamba zikashamiri magugu, nyua zikaachiliwa, na hivyo wanyama wakakosa chakula cha kuwatosha. Baada ya kukaa wikendi nzima bila kitafunio, wanyama wanaamua kuvunja desturi na ng’ombe mmoja anafaulu kuuvunja mlango wa ghala kwa kutumia pembe. Hili linawanufaisha wanyama wote; wanaingia ghalani na kula chochote walichojaliwa kupata. Baada ya binadamu – anayeashiriwa na Bwana Mtiki na wafanyakazi wake wanne – kushindwa kuwafukuza wanatoroka. Jambo hili linakuwa kilele cha mapinduzi na kuzalisha mwanzo mpya pale shambani. Haya yote yanafanikishwa kupitia matumizi ya mbinu ya anthropomofiki. Viongozi

wengi Barani Afrika hulewa mamlaka. Hili huwafanya kufanya mambo kiholela kama kutoa leseni ovyo za ukataji miti na ujenzi kwenye maeneo oevu; suala ambalo husababisha unajisi wa mazingira kwa ujumla.

Mapinduzi hayakuwa rahisi kuyaratibu na kuyatayarisha. Kianthropomofiki, nguruwe wanasawiriwa kama waliowajibika kupanga na kufanikisha mapinduzi. Walipanga mpango wa unyama juu ya mafundisho ya Mbalamwezi katika mfuatano wa mawazo kamili. Baadhi ya wanyama walisisitiza uaminifu wao kwa Bwana Mtiki kama mtawala wao. Hili linaashiria jinsi baadhi ya viongozi wanavyoamini na kuwajibikia mabeberu badala ya kuwawajibikia wananchi wao. Mathalani, wanyama wengine wanadai, "Bwana Mtiki huwalisha. Iwapo angekwenda, wangekufa kwa njaa" (uk. 18). Hili linaashiria jinsi baadhi ya viongozi kama Chifu nyakati za m-beberu na hata katika kipindi cha ukoloni mamboleo wanavyomtegemea m-beberu kuwapa chakula. Chakula hiki huja kupitia mikopo yenye riba kubwa. Hali hii huimarisha utumwa na utegemezi wa mataifa duni kwa yale yenye ukwasi.

Waithiru (2019) akimnukuu Thiong'o (1987) anaeleza kuwa mkoloni alipofika katika Bara la Afrika, mkono mmoja alishika Biblia ilhali wa pili alibeba bunduki. Hivyo, kupitia ukoloni mamboleo unaoashiriwa na bunduki, mkoloni hadi leo hulitawala Bara la Afrika kupitia ukoloni mamboleo. Aidha, alitumia Biblia kuudhalilisha utamaduni wa Mwafrika na ingawa hakuuondoa kabisa, uliweza kunajisiwa kupitia uhuluti, ukaweza kuzalisha utamaduni ambao badala ya kumpa Mwafrika utambulisho humpa utumwa kamili (Njeru, Kobia na Musyimi, 2022).
Hii ndiyo sababu baadhi ya wanyama hawakuona haja ya kujishughulisha na mambo ambayo yangetokea baada ya wao kuaga dunia. Sukari anayodai Mjinga inaashiria baadhi ya misaada inayotolewa na mashirika mbalimbali ya kimataifa kwa mataifa fukara ya Afrika. Mjinga anauliza ikiwa ataendelea kupata sukari baada ya mapinduzi, na ikiwa atapewa ruhusa ya kuendelea kuvaa utepe. Hili linaashiria kuwa utepe wanaovalishwa mataifa fukara ya Afrika na yale tajiri ya Ulaya unawapofusha na kuwapumbaza Waafrika. Utepe huu ni mikopo na ufadhili wa miradi isiyo na umuhimu kwa wananchi. Mawazo ya Thiong'o (1987), Maathai (2009), Iheka (2015) na Waithiru (2022a) yanaungana na watafiti kuwa, Mwafrika ni mtumwa wa ufadhili na mikopo ya kulazimishwa yenye masharti ya kiutumwa na riba ya kulemaza chumi za Afrika. Orwell anathibitisha hili anapoeleza:

> "Baada ya siku tatu, Mjinga alitoweka kabisa. Kwa muda wa majuma matatu, hakuna aliyekuwa na habari zake. Baadaye njiwa … walimwona … Alikuwa amebebwa katika gari lililosimama nje katika hadhara ya watu. Mtu … mtoza ushuru, alikuwa akimlisha mapande ya sukari. Koti la Mjinga lilishonwa upya, pia alijizungusha utepe mwekundu … (uk. 43).

Kadhalika, Jurawa-kunguru analemaza harakati za mapinduzi kupitia tuhuma za uongo. Tuhuma hizi zinaashiria dini aliyotanguliza m-beberu Barani Afrika ambayo

haikuwa sehemu ya utamaduni wa Mwafrika. Mwandishi Orwell anafanikisha haya kupitia anthropomofiki. Jurawa alidai kuwa alimaizi nchi ya ajabu iliyoitwa Mlima Halua ambapo wanyama walienda baada ya mauko yao. Huko siku zote saba za wiki zilikuwa Jumapili. Hadithi za Jurawa zilikuwa kizingiti katika shughuli za mapinduzi lakini hazikufana madhali nguruwe walitambuliwa na wanyama wengine wote kama walimu wao. Baada ya Mtiki na wafanyakazi wake wanne kushindwa kuwadhibiti wanyama, wanatoroka na kulikimbia Shamba la Ibura. Vita kati ya wanyama na wanadamu vinaashiria vita vya uhuru vya mataifa ya Afrika kutoka kwenye utawala wa m-beberu. Mapinduzi, hivyo, yanaashiria vita vya uhuru wa Afrika. Maelezo haya yote yanafanikishwa na mwandishi kupitia anthropomofiki. Kiuyakinifu, wanyama hawakuwa wamenuia kutekeleza mapinduzi ila kutokana na dhuluma za binadamu walishindwa kuvumilia na wakawafukuza watu kutoka mle shambani.

Vifaa vilivyotumbukizwa kisimani na vingine kwenye shimo la takataka kama vile hazama, minyonyoro ya mbwa, lijamu, visu vikali vilivyotumiwa na Bwana Mtiki kuwachinja nguruwe na ndama, hatamu, kamba, vidato na mifuko ya pua vinaashiria utumwa. Utumwa huu ulikusudiwa kufifishwa baada ya vita vya uhuru wa mataifa ya Afrika kufana. Hata hivyo, kupitia ukoloni mamboleo, utumwa ungali upo (Alia, 2017; na Waithiru, 2019). Mzushi alizichoma tepe zake kuashiria mwanzo mpya wa uhuru wa wanyama. Walipoona vifaa vile pamoja na mijeledi ikiungua motoni, walisherehekea kwa shangwe na vigelegele. Mzushi anadai kuwa wanyama wanapaswa kutembea uchi kuashiria Uafrika na uhuru ila si mavazi kama tepe zinazoashiria ukoloni peupe. Siku waliyoupata uhuru, wanyama walilala usingizi mtamu kuliko siku nyingine yoyote. Uhuru wa binadamu huzalisha uhuru wa kimazingira. Wanyama baada ya kujinyofoa kutoka kwenye minyororo ya utawala dhalimu wanayanadhifisha mazingira na kutumia mbinu asilia za kilimo badala ya kemikali sumu.

**4.4 Elimu**

Muriithi (2017) anafafanua kuwa elimu ni namna ambayo hutumiwa kwa lengo fulani na jamii kupitisha maarifa, utaalamu, utamaduni, ujuzi na maadili kutoka kwenye kizazi kimoja hadi kingine. Kwa upande mwingine, elimu ni uzoefu wenye athari ya kujenga akili, hulka, au/ na uwezo wa kimaumbile wa mtu binafsi. Hii ni kwa sababu, kila jamii huwa na upekee wa kimwonoulimwengu, mifumo na miundo yake maalum (Muhia, Mwamzandi na Kisurulia, 2019). Mtunzi Orwell kwa kutumia anthropomofiki anadhihirisha jinsi elimu inavyochangia kukabiliana na ufukara, uongozi mbaya, kuimarisha taasisi mbalimbali, amani, undugu na umoja katika jamii. Nguruwe, wakiongozwa na Mzushi, wanawaonesha wanyama wengine kuwa kwa muda wa miezi mitatu iliyopita wamekuwa wakijifunza kusoma na kuandika. Ingawa si kawaida wanyama kusoma na kuandika, mwandishi anasawiri kupitia anthropomofiki, hali hiyo ambapo wanyama wanaendeleza utawala mpya kwa kuongozwa na elimu. Kitabu walichokitumia nguruwe kiliwahi kutumiwa na

watoto wa Bwana Mtiki. Walikuwa wamekitoa kutoka kwenye lundo la takataka kuashiria uharibifu wa mazingira ya watawaliwa na watawala. Hili linaashiria kuwa, ingawa m-beberu ana elimu, Waafrika wanaweza kutumia elimu ileile kujiendeleza wao wenyewe bila kutawaliwa na m-beberu huyo.

Mabadiliko ya kwanza yanafanikishwa na wanyama kupitia elimu ili kubadili utambulisho wao. Mzushi kwa kutumia makonzi ya mguu wake alichukua burashi na akafuta kabisa maandishi ya SHAMBA LA IBURA kwenye lango na badala yake akaandika kwa uangalifu sana:, SHAMBA LA WANYAMA. Hili likawa jina jipya la shamba kuanzia siku hiyo. Hivyo, mwandishi anaashiria kuwa Mwafrika ana uwezo wa kujitambua mwenyewe bila kutegemea utambulisho anaopewa na mkoloni, unaomdhalilisha kwa kila hali kupitia utamaduni mpya. Hili linawiana na kauli ya Howarth (1996) kuwa, utamaduni na mazingira huwa na uhusiano wa kisimbiyotiki ambapo hukamilishana. Ingawa utamaduni wa Mwafrika huwa na mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, utamaduni wa mkoloni hupalilia unajisi wa mazingira (Ballard, 2023). Muhia, Mwamzandi na Kisurulia (2019) wanaungana na watafiti kuwa elimu ni ala nzuri na mwafaka ya kujikomboa kutoka ukoloni mamboleo Barani Afrika, ikiwa itamulika changamoto na dhiki za Afrika badala ya kuangaza maslahi ya mabeberu wa kisasa. Wanaongeza kwamba elimu katika nchi za Afrika humtayarisha mwananchi kutegemea serikali na hivyo huzalisha utegemezi badala ya mwananchi kujitegemea kistadi, kimawazo, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hivyo, Mwafrika atapata uhuru kamili, wakati elimu yake itakapoangaza uzalishaji wa suluhu, ila sio kutibu dalili huku chanzo twakipalilia.

Kadhalika, kwa kutumia anthropomofiki, mwandishi Orwell anaonesha haja ya kuwapo kwa katiba katika nchi ili watu waishi kwa kufuata utaratibu fulani. Wanawafahamisha wanyama kuwa mafunzo waliyojipatia kwa muda wa miezi mitatu yaliwawezesha kufaulu kufupisha kaida za Unyama katika kanuni saba. Sheria zile saba zilikuwa katiba ya wanyama ya kuwakumbusha jinsi ya kuishi, kila mmoja na mwingine, huku wakizingatia unyama. Kwa shida, Mzushi anapanda juu na kuziandika huku Mcheshi akishika kopo la rangi kumrahisishia kazi. Ziliandikwa pale ukutani kwa herufi kubwa. Sheria hizi zilidhihirisha bayana sifa za adui na namna ya kuvaa na kuishi mle katika Shamba la Wanyama. Sheria iliyopewa uzito ni ya saba iliyoeleza kuwa, “Wanyama wote wako sawa” (uk. 25). Kupitia anthropomofiki, haya yote yanafanikishwa na pia nguruwe wanaweza kuwakama ng’ombe vyema. Aidha, viongozi katika mataifa yanayoendelea huwatumia wananchi kama watumwa. Kupitia utozaji ushuru wa juu zaidi bila huduma wala matumizi yenye uwajibikaji ya kodi hiyo; huwanajisi wananchi na kuyafanya mazingira yao kuwa tasa kutokana na uharibifu.

Ingawa Mzushi na Mkimwa hawakuelewana kwa lolote, walitumia chumba kilichotumiwa kuhifadhi lijamu na vigwe kujifunza stadi aina aina, kama vile uhunzi, useremala, na ufundi mwingine tofauti, kutoka kwenye vitabu vilevile

walivyovipata. Elimu inamsadia Mzushi kuwatenga wanyama katika vikosi tofautitofauti alivyoviita Halmashauri za Wanyama. Kwa mfano, alianzisha halmashauri ya utagaji wa mayai kwa kuku, chama cha kukagua usafi wa mikia ya ng'ombe, ya kuwahekimisha wanyama wasiofugwa na halmashauri zingine kadhaa. Mwandishi anasisitiza, "Masomo ya kuandika na kusoma yalifaulu sana. Kabla ya masika, karibu kila mnyama aliweza kuandika na kusoma kwa kiasi fulani" (uk. 31). Hivyo, elimu kando na kuboresha njia madhubuti za uhifadhi wa mazingira kupitia njia bora za ukulima, huwaleta viongozi wenye misimamo kinzani pamoja.

Anthropomofiki imetumiwa na mwandishi kufanikisha mapinduzi kupitia elimu kwa njia inayoburudisha na kuvutia. Mathalani, Mjinga aliweza kujifunza herufi sita zilizokuwa zinaandika jina lake. Punde tu alipofaulu kuziandika, alikuwa anaziashiria kupitia vipande vya matawi aliyoyatumia kusawiri ardhini. Hali hii inasawiri namna ambavyo ujinga husherehekewa katika mataifa duni ulimwenguni. Baada ya Mjinga kuzisawiri alizipamba kwa ua moja au mawili na hatimaye, angezunguka kwa madaha huku akizistaajabia. Kwa misingi hiyohiyo, kujifunza herufi zote lakini hakuweza kuzitumia kuunda leksia kamili. Elimu hii inawawia ngumu baadhi ya wananchi katika mataifa tofautitofauti ulimwenguni. Inapalilia uchafuzi wa mazingira badala ya uhifadhi. Hii ni kwa sababu, kusudi kuu la elimu hii ni kuwapofusha wananchi hasa Waafrika na kuwapumbaza bila kuzishughulikia changamoto zinazowakabili kila uchao.

Mwenge kwa upande mwingine, alifaulu kuelewa herufi nne tu kwa wakati mmoja. Hii inamaanisha kuwa angejifunza herufi nne tofauti leo, kesho tena zingine tofauti; ubongo wake ungesahau za mwanzo na kukumbuka za wakati huo. Ingawa malengo ya elimu katika mataifa mengi yaliyowahi kutawaliwa na mkoloni ni mwafaka, elimu yenyewe huwa inapalilia utegemezi, utumwa na upofu bila kuzalisha uzinduzi na ubunifu katika kuyasuluhisha matatizo yanayowakumba wananchi hasa ya kimazingira. Mathalani, Orwell anaeleza:

> Kwa kutumia ukwato wake mkubwa aliweza kuandika mchangani herufi A, B, C, D,. halafu alisimama na kuziangalia, masikio yake yakisimama wima, akijitahidi kukumbuka herufi zilizofuata bila kufaulu. Wakati mwingine aliweza kujifunza E, F, G, H, lakini alipozijua, alijikuta ameishasahau A, B, C, na D (uk. 32).

Mlikuwa na wanyama kama kondoo, kuku na bata ambao walishindwa kujifunza wala kuzikumbuka sheria zile saba. Hili lilimpa Mzushi sababu ya kuzifupisha sheria saba zikawa moja iliyoeleza kuwa, "Miguu minne ni mizuri, miguu miwili ni mibaya" (uk. 32). Ingawa alisingizia kisababu cha kufupisha kama kuwasaidia wanyama wajinga kuelewa, alikuwa na nia ya kuwatawala wale wajinga. Hili linaashiria viongozi Waafrika ambao huwatumia Waafrika wenzao kama vifaa vya

majaribio ya chanjo tofautitofauti kutoka ughaibuni (Waithiru, 2019; Waithiru na wenzake, 2021).

**4.5 Ubepari**

Kupitia mhusika Mkimwa, mwandishi anadhihirisha athari za ubepari katika nchi za Afrika kwa kutumia anthropomofiki. Mkimwa anavunja sheria za wanyama saba kutokana na ubinafsi wake wa kujitajirisha mwenyewe bila kuwajali wanyama wengine. Marx (1867) anaeleza kuwa, ubepari ni hali ya uchumi wa kuwezesha watu wachache kuwa na mali nyingi na kumiliki uchumi wa nchi. Umiliki huu hulindwa kwa kuwaangamiza washindani na kuwanyamazisha wenye uwezo wa kuwa wapinzani. Nguruwe wakiongozwa na Mkimwa ndio wanaomiliki mali nyingi pale Shambani. Wamitila (2003) na Peterson (2022) wakikubaliana na mawazo ya mtafiti wanasema kuwa, ubaguzi na ubepari ni suala linalochipuza chimbuko lake katika mizizi ya ubaguzi wa rangi. Ingawa wanashikilia kuwa ubaguzi ulipata mashiko kutokana na haja ya Mwingereza kutaka kuhimili na kudhibiti ulimwengu, wanaongeza kuwa ni suala linalozua migogoro ainaaina katika jamii.

Wanyama waliokuwa wameapa kutoshirikiana na binadamu wanamkaribisha Bwana Msuluhishi kila Jumatatu pale katika Shamba la Wanyama kupokea mahitaji ya wanyama. Mcheshi anatumiwa na Mkimwa kuwahakikishia wanyama kuwa mambo yalikuwa sawa. Ingawa uhusiano kati ya wanyama na binadamu umegubikwa na ulaghai na maonevu, wanyama walipomuona Bwana Msuluhishi akipewa maagizo na nguruwe, huku nguruwe akiwa amesimama kwa miguu minne na Msuluhishi kwa miguu miwili, walifurahia sana mpango ule mpya na wakausifu ghaya. Kutokana na ubepari mwandishi anaeleza kuwa, "Sasa uhusiano wao na binadamu ulihitilafiana kwa mbali na ule wa siku zilizopita" (uk. 59). Kando na fununu za Mkimwa kufanya biashara na Bwana Taanasa wa Chaka au Bwana Chagina wa Siha, nguruwe walihamia katika nyumba nzuri iliyowahi kuwa ya Bwana Mtiki. Wanyama walipolalamika, Mcheshi aliwahimiza kwa upole kuwa, "… ilikuwa halali kwa nguruwe, viumbe waliokuwa bongo za shamba, kupata nafasi ya faragha waweze kufanya kazi zao iwapasavyo" (uk. 59). Hili linaonesha jinsi viongozi wanavyofanya mipango kwa manufaa yao bila kuwajali wananchi. Mcheshi anataja kuwa, kiongozi kama Mkimwa hafai kuishi katika zizi bali katika nyumba nzuri. Hili linadhihirisha jinsi viongozi wengi Barani Afrika huyatumia mataifa yao kujipa nafasi, utajiri na mali kisha huyadharau pamoja na wananchi kwa ujumla. Zizi linalorejelewa linasawiri makazi ya wananchi wengi duni katika mataifa mengi ulimwenguni, hususan ya Afrika. Hali hii inafungamana na mhimili wa uwezo na kifo wa Nadharia ya Uhakikimazingira ambapo viongozi wenye mamlaka pamoja na matajiri hutumia rasilimali asilia, ushuru unaotolewa na wananchi pamoja na juhudi za wananchi katika ujenzi wa taifa kujinufaisha huku wakiyanajisi mazingira.

Nguruwe wanawatapeli wanyama wenzao kimawazo ili kujitajirisha. Mcheshi anawaeleza Mbio, Kadiri na wanyama wengine wote kuwa, "Sheria ilizuia 'mashuka' ambayo ni uvumbuzi wa binadamu. Tumeyahamisha mashuka yote kusudi tulale kati ya blanketi tu" (uk. 60). Viongozi matapeli hubadili msimamo ili kutegemea ule unaowanufaisha wao bila kuwajali wananchi. Mathalani, Mkimwa akisikizana na Taanasa, anawaambia Njiwa wabadili usemi. Anawaeleza kuwa, "… usemi wa "Binadamu alaaniwe", uwe, "Chagina alaaniwe" (uk. 82). Lakini punde tu Taanasa anapotoa fedha nyingi kununua mbao za Mkimwa kuliko Chagina, Mkimwa anawaamuru Njiwa kubadili wito na kusema kuwa, "Taanasa alaaniwe," (uk. 83) badala ya "Chagina alaaniwe" (uk. 83). Mbao anazouziwa Taanasa na Mkimwa (kiongozi nguruwe) zinasawiri hali halisi katika mataifa duni duniani. Viongozi wa mataifa yanayojiendeleza huyapujua mazingira yao kwa manufaa yao bila kujali madhara yake kwa mazingira katika siku za usoni.

Viongozi wanaoongoza ubepari Barani Afrika hulaghai katika ndoa na huishia kuwa na Masuria wengi ambao wakati mwingine huwazalisha watoto. Usaliti huu wa ndoa huwa mwendelezo wa usaliti wa uongozi na wa taifa kwa ujumla. Jambo hili huwapa viongozi hawa msukumo wa kutumia mali ya umma kwa manufaa yao pamoja na jamaa zao. Mathalan, Mkimwa anazalisha nguruwe jike wanne wanaozaa jumla ya watoto 31. Mkimwa anaagiza kununuliwe matofali na mbao vya kujenga chumba kidogo cha kusomea pale bustanini. Ujenzi ukiendelea, Mkimwa alilitumia jiko kama darasa la nguruwe wake wachanga. Hili linaashiria jinsi viongozi Barani Afrika hutumia mali ya umma kuwaelimisha watoto wao katika shule za kifahari bila kuwajali wananchi fukara na watoto wao. Mwandishi anataja kuwa, "Walipewa mazoezi ya viungo faraghani pia walizuiwa kucheza na watoto wa wanyama wengine" (uk. 94). Haya yote, mtunzi Orwell anafanikiwa kuyasawiri kupitia anthropomofiki.

Viongozi ambao hupalilia ubepari huulinda kwa hali na mali. Kiongozi Mkimwa (nguruwe), kwa mfano, anahakikisha kuwa nguruwe wengine hawapati hata punje moja ya sukari. Mwandishi anathibitisha hili anaposema, "… hata sukari ilitumiwa na Mkimwa peke yake (hakuwaruhusu nguruwe wengine kuitumia sababu ati iliwanenepesha mno) …" (uk. 94 – 5). Ubinafsi, tamaa na ufisadi vinadhihirika pale ambapo nguruwe wanakosa tatizo na zaidi wanaendelea kunenepa zaidi kila siku. Kwa wakati huo wanyama wengine waliendelea kuteseka kwa njaa kwa sababu pishi zilizidi kupunguzwa. Wanyama wengine wakiendelea kudhoofika kiafya, nguruwe wakiongozwa na kiongozi Mkimwa waliendelea kushiba na kujifariji kwa kibaba cha pombe kila siku. Kiongozi Mkimwa alikuwa na haki ya pishi mbili zilizojazwa kutwa na kupakuliwa kwa kombe lake la gharama kubwa. Hakika, ubinafsi wa viongozi katika mataifa duni husababisha utabaka na ubaguzi kwa kiwango kikubwa.

Nyimbo na ushairi ni baadhi ya ala ambazo hutumiwa kudumisha ubepari Barani Afrika. Mathalani, wakati wa wanyama kuandamana na kuzunguka kijeshi shamba zima, Mwenge na Mbio waliinyanyua juu bendera ya kijani iliyochorwa ukwato na pembe yenye maandishi yaliyosema, "Ndugu Mkimwa aishi milele!" (uk. 96). Kwa misingi hii, mashairi yaliyotungwa kumsifu kiongozi Mkimwa yanapalilia ubepari. Kwa mfano, Orwell anaeleza, "Mashairi yaliyotungwa kwa heshima yake yaliimbwa". (uk. 96). Katika mataifa yanayoendelea viongozi huwapumbaza wananchi na nyimbo za ulaghai ambazo huwasifu kutokana na vitendo visiyo vya kweli ila vya kifantasia tu. Wananchi nao kwa kweli huuamini ulaghai huo na huishia kujilaumu kila baada ya uchaguzi. Inaumiza kujiuliza ni lini wananchi watawachagua viongozi kwa mujibu wa sera, utendakazi na uwezo wao katika kuyashughulikia matatizo ya taifa husika.

Viongozi hawa hutumia dini kama ala ya kuwatuliza wananchi maskini, kuwapumbaza na kuwapa matumaini kuwa wasifadhaike kwani Mlima Halua mna raha bila mwisho wala isiyomithilika. Kupitia mhusika Jurawa, mwandishi anathibitisha hili. Jurawa alikuwa anatulia kiotani mwake na kumsimulia mnyama yeyote ambaye alielekea kumsikiliza. Jurawa ni taashira ya wahubiri, mashehe, na makuhani mbalimbali katika nchi za Afrika ilhali kiota chake ni taashira ya kanisa, misikiti na vyumba vingine vya kuabudia. Hakika, viongozi wengi hasa wa Afrika hutumia simulizi za uongo kuwapa wananchi matumaini matupu huku wakitenda kinyume kwa kuendelea kuyadidimiza mazingira yao kwenye maangamizi huku wakiyafanya mataifa yao maabara ya majaribio ya chanjo ainaaina za mataifa tajiri ya Uropa, Marekani, Uchina na kwingineko. Hili linafungamana na kauli ya Oliver (2016) kuwa, mataifa mengi yanayoendelea hutumiwa kama maeneo ya majaribio na viongozi wa mataifa yaliyowahi kuyatawala enzi za ukoloni mkongwe na ambao huendelea kuyatawala katika istilahi ya kitasfida ya utandawazi. Thiong'o (1987) anaongeza kuwa viongozi wa mataifa haya duni hupalilia upofu wa wananchi kwa kutumia dini waliyoachiwa na mkoloni. Jurawa alikuwa akielekeza mdomo wake mkubwa juu na kusimulia:

> Juu kule, Ndugu yangu, juu kule, upande wa pili wa Wingu hilo ulionalo ndipo palipona nchi hiyo ya furaha, mahali ambapo sisi wanyama fukara tutaenda kupumzika baada ya kazi zetu nzito! (uk. 97).

Kazi kubwa ya Jurawa ilikuwa kukaa bila kufanya kazi na kuhadithia hadithi zilizohusiana na Mlima Halua. Aliwadanganya wanyama kuwa yeye mwenyewe aliwahi kufika huko na kushuhudia uzuri wa eneo lile. Aliripoti kuwa mashamba ya Mlima Halua yalipambwa kwa maua aina tofautitofauti ambayo licha ya kuyapamba mashamba, yalikuwa lishe bora kwa ng'ombe. Kadhalika, mlikuwa na mikate mitamu iliyotayarishwa kwa kuchanganywa na mbegu za katani. Vibonge vya sukari navyo vilioteshwa kwenye nyua. Ulaghaai unaoendelezwa na viongozi

wa dini katika mataifa duni unaimarisha uongozi mbaya na hatimaye kupalilia ubepari wa kisasa, utegemezi na utumwa wa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Viongozi katika mataifa duni wanatumia mali ya umma kwa manufaa na raha zao. Mathalan, nguruwe wananunua sanduku la pombe na kusherehekea kifo cha shujaa Mwenge. Pesa wanazotumia nguruwe kununua sanduku la pombe zinatokana na malipo yaliyotolewa na Katoki, mchinja farasi na mchemsha gundi aliyemnunua Mwenge. Mwandishi anataja kuwa, "Mnong'ono ulizidi kuenea kwamba nguruwe walijipatia pesa zaidi kutoka mahali fulani za kununulia sanduku lingine la pombe" (uk. 104). Hakika hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo na kifo ambapo baada ya viongozi kuwatumia wananchi bila kuwapa huduma bora za afya, wananchi huangamia na badala ya viongozi hawa kuhuzunika wao husherehekea. Kwa kweli ushenzi na upofu ulo katika mataifa haya ni wa kutamausha. Linalosalia mawazoni mwa wengi ni je, ni lini wananchi watajizoazoa kutoka kwenye giza la utumwa, mazingira chafu na minyororo ya mabepari kwa ujumla?

Mwandishi anasisitiza kuhusu ubepari kianthropomofiki katika Shamba la Wanyama kwa kuwasawiri viongozi na walinzi wao wakinufaika huku wananchi wakiumia. Hili analifanikisha anapotaja kuwa, "Ilielekea shamba lilitajirika pasipo kuwatajirisha wenyeji wake bali nguruwe na mbwa" (uk. 107). Katika ubepari, wananchi huendelea kuhimili njaa, matatizo na machukizo ambayo ni sheria ya maisha yasiyobadilika. Kondoo wanatumiwa kufanikisha ubepari kwa kuwatukuza viongozi dhalimu, binafsi na wenye tamaa kama kiongozi Mkimwa na Mcheshi. Baada ya nguruwe kufanikiwa kutembea na miguu miwili, kondoo wanabadili wimbo. Hapo kabla walikuwa wanaimba kuwa, "Miguu minne ni mizuri, miguu miwili ni mibaya" (uk. 50). Kondoo ni taashira ya wananchi waoga, wabinafsi na wajinga ambao huwasifu viongozi wanaopalilia ubepari katika nchi za Afrika. Baada ya nguruwe kutembea kama binadamu, kondoo wanaanza kuimba kuwa, "Miguu minne ni mizuri, miguu miwili ni mizuri zaidi!" (uk. 110). Hili linaashiria wananchi na wafuasi waaminifu wa viongozi bepari Barani Afrika. Hili linashabihiana na nguzo ya uongozi mbaya na ukoloni mamboleo ambapo viongozi wanaodhibitiwa kama vikaragosi na viongozi wa mataifa yenye uwezo huwalaghai wananchi wao, na huyasaliti mazingira yao kwa manufaa ya watawala wao.

Mtunzi Orwell anahitimisha suala la ubepari kwa kusawiri ukosefu wa usawa kati ya wenyeji katika mataifa yanayoendelea. Ukosefu huu wa usawa licha ya kuhusisha ukosefu wa usawa wa kijinsia hujikita sana katika ubaguzi wa kimazingira, kisiasa, kijamii na hasa kiuchumi. Kwa mfano, mwandishi anataja kuwa:

> WANYAMA WOTE NI SAWA
> LAKINI BAADHI YAO
> WAKO SAWA ZAIDI YA WENGINE (uk. 111).

Kauli hii inaunganisha na kujumlisha kwa msisitizo mihimili yote miwili iliyoongoza tathmini ya makala haya. Mihimili ya uwezo na kifo, na uongozi mbaya na ukoloni mamboleo ndiyo inayozalisha kauli kama hizi ulimwenguni. Hakika, katika mataifa mengi Barani Afrika, hali hii hukumbatiwa, hupigwa busu na kuabudiwa na watawala pamoja na watawaliwa mtawalia. Hali hii husababisha unajisi sio tu wa mazingira halisi, pia wa kimawazo na wa maadili. Nadharia ya Uhakikimazingira inakemea mawazo mgando na potofu kama haya kupitia mihimili ya uwezo na kifo, na uongozi mbaya na ukoloni mamboleo na badala yake kusisitiza haja ya kuyahifadhi mazingira asilia; kuboresha uongozi bora; kujitegemea; usawa na haki sawa kwa wote huku suluhu zikitafutwa kutoka kwenye mazingira yenye tatizo badala ya kutoka ugenini.

**4.6 Uongozi Mbaya**

Uongozi mbaya unazalisha woga baina ya wanyama pale shambani na hatimaye maafa. Kwa misingi hii, uhakiki wa kipengele hiki uliongozwa na mhimili wa uongozi mbaya na ukoloni mamboleo wa Nadharia ya Uhakikimazingira. Uongozi mbaya husababisha ongezeko la uzalishaji wa gesi chafu kutokana na viwanda ambavyo huruhusiwa na utawala dhoofu kutekeleza shughuli zao bila kujali madhara yake kwa watu na mazingira kwa ujumla. Mabadiliko ya tabianchi ambayo hutishia afya ya binadamu, viumbehai, pamoja na mifumo ya ekolojia hushamiri. Shughuli hizi hutekelezwa na mashirika tajiri katika mataifa yanayoendelea bila upinzani kutoka kwa yeyote. Kimya hiki hukithiri kutokana na woga wanaotiwa wananchi na viongozi wa mataifa yao. Woga huu huimarishwa kupitia vitisho na maangamizi ya wapinzani na wazalendo. Katika Shamba la Wanyama kwa mfano, baada ya siku nne kupita, majira ya jioni, Mkimwa aliamuru wanyama wote wajumuike uani. Walitii na kila mmoja akajipa nafasi yake. Mkimwa aliposimama kuzungumza, alitoa mlio mkali na mara mbwa waliwarukia nguruwe wanne na kuwang’ata masikio. Baada ya kung’atwa masikio waliburutwa na kulazwa mbele ya kiongozi Mkimwa. Hii ni taswira ya mambo halisi katika nchi za Afrika. Kule kuonja kwa damu ya nguruwe wale wanne na wale mbwa wa Mkimwa kunaashiria jinsi ambavyo vitengo vya usalama hutumiwa na viongozi kuwanyanyasa wapinzani kisha askari wanaotumiwa kuwatesa huwaibia wapinzani wale mali na haki zao. Wale mbwa watatu wanaomwendea Mwenge (farasi) wanasawiri unyanyasaji wa wapinzani wa serikali na utawala. Hata hivyo, Mwenge anawasawiri wananchi wachache wenye uwezo wa kiuchumi na mali wanaojua na kuweza kupigania haki zao. Hata hivyo, kuna haja ya kuwahamasisha wengi kuhusu haki za binadamu na za mazingira ili kuimarisha ujasiri, udadisi na uzalendo na kukemea woga.

Mkururo wa wanyama wengi waliotubu kuhusu mambo mbalimbali yaliyokuwa kinyume na imani na sera za uongozi wa Mkimwa uliuawa. Maangamizi huwa ala kwa viongozi wa mataifa duni ya kuwahakikishia utawala usio na pingamizi; hivyo wao hutende wapendavyo bila uwajibikaji wowote ule. Wanyama waliangamizwa

hadi mkawa na mlima wa maiti za wanyama waliochinjwachinjwa mbele ya Mkimwa. Hili linawiana na hali halisi katika mataifa duni ulimwenguni. Katika mataifa haya viongozi huchangia uchafuzi kwa kuwaangamiza wanaowapinga kisera, kisiasa, kiuchumi na hata kijamii. Waithiru (2019: 102) anaeleza kuwa: uchafu huu unatokana na siasa mbaya na upotofu wa maadili. Huu ni uhalisi katika mataifa mengi fukara ambapo wenye uwezo huwaangamiza wanyonge pamoja na mazingira yao.

Hewa ilinajisiwa na harufu nzito ya damu ambayo ilihanikiza hadi nje ya Shamba la Wanyama. Huu ni uchafuzi wa mazingira katika nchi zisizo na mfumo thabiti wa utawala na uzingativu wa sheria. Hili halikuwahi kutokea hata wakati Bwana Mtiki alipokuwa anatawala pale shambani. Mwandishi anaeleza kuwa, "Katika siku za zamani, palikuwepo pia umwagikaji wa damu, lakini huu uliofanyika, ulionekana kwa wote kuwa mbaya zaidi, maana ulitokea kati yao wenyewe" (uk. 73). Viongozi wengi waliochukua hatamu za mamlaka baada ya m-beberu kuondoka walifuata nyayo zilezile za m-beberu. Hata hivyo, baada ya miongo kadhaa viongozi waliomo wamezipiku nyayo zile na kupiga hatua kuinua kiwango cha uovu, dhuluma, maonevu na unajisi wa mazingira. Hili huchangiwa sana na ukweli kwamba wengi hukatalia mamlakani kwa miongo mingi. Hali hii ingawa imefanikishwa kwa kusawiriwa kupitia anthropomofiki inaakisi hali halisi katika mataifa mengi Barani Afrika ambapo viongozi hutawala zaidi ya miongo miwili mtawalia.

Katika kipindi cha ukoloni mamboleo, Waafrika wanauawa kisiasa, kiuchumi na hata kijamii pamoja na kunyang'anywa uhai wao. Hiki nii kipindi ambacho uongozi dhalimu unashamiri na watu kunyimwa haki hadi ya kujieleza. Kwa mfano, Mbio anajiuliza kuwa, "Hakuelewa kwa nini – waliufikia wakati ambao uliwafanya wanyama waogope hata kutoa mawazo yao – wakati ambao majibwa makali yangurumayo yalienea kila mahali, na kuwaona ndugu zao wakiraruliwa baada ya kuyaungama makosa yao…" (uk. 74). Ingawa mataifa mengi Barani Afrika yalipigania uhuru wao na hakika wakaupata, bado yangali yanaongozwa kupitia njia zilezile za m-beberu, zinazojaa mateso, udhalimu, maafa, maradhi na ufukara.

Wanyama walipompiga na kumfukuza m-beberu – Bwana Mtiki – walipandisha hata bendera. Mwandishi anathibitisha hili anapotaja kuwa, "Zilifuata sherehe zilizoandaliwa kuutukuza ushindi. Bendera ilipandishwa na wimbo wa *Ndugu Zangu e Wanyama* uliimbwa mara kadhaa" (uk. 40). Kutokana na woga wa wananchi wa kutawaliwa na m-beberu tena, wao huendelea kukuza na kupalilia uongozi mbaya kutokana na ufukara wa kimawazo, kihisia na kiuchumi. Mtunzi Orwell kupitia mhusika Mbio anaeleza kuwa, "Hata kama ingetokea nini, angeendelea kuwa mwaminifu, angefanya kazi kwa bidii, angetii amri alizopewa pamoja na kuukubali uongozi wa Mkimwa" (uk. 75). Kupitia uongozi wa kidikteta, Mcheshi anawajuza wanyama kuhusu amri ya Mkimwa iliyosema kuwa wimbo wa *Ndugu Zangu e Wanyama* ulikuwa marufuku kuimbwa tena. Mcheshi aliwaeleza

kuwa sababu na kusudio la wimbo lilikuwa kupata ustawi wa siku zijazo ambao walikuwa nao chini ya uongozi wa Mkimwa, na hivyo hakukuwa na haja tena ya kuuimba. Hili ni uthibitisho kuwa uongozi mbaya hubabaishwa na udugu na umoja wa wananchi.

Chini ya utawala dhalimu, viongozi hubatili sheria kwa manufaa yao. Mathalani, Mkimwa kwa kumtumia Mcheshi, anabadili sheria ya sita. Kabla ya kubadilishwa, Sheria ya Sita ilisema kuwa hakuna mnyama yeyote aliyeruhusiwa kumwangamiza mnyama mwingine. Hata hivyo, ilibadilishwa kwa kuongezwa maneno zaidi bila kushirikishwa wala kuhusishwa kwa wanyama waliotawaliwa na sheria hiyo. Ilibadilika na kusema kuwa, "Mnyama yeyote asimuue mnyama mwingine bila sababu" (uk. 77). Ingawa wananchi huogopa kurejea kwa m-beberu na hivyo kuvumilia uongozi mbaya, mara nyingi mateso ya viongozi Waafrika kwa wananchi hupiku yale yaliyokuwa ya beberu.

Viongozi wanaoendeleza uongozi mbaya hubadili msimamo na kuegemea ule unaowafaa wao. Mathalani, Mkaidi aliwasomea wanyama wengine maandishi yaliyokuwa yameandikwa ubavuni mwa gari lililombeba Mwenge yaliyosema kuwa, "Katoki mchinja farasi na mchemsha gundi. Mchuuzi wa ngozi na matundu ya mbwa!" (uk. 101). Lakini, Mcheshi baada ya maafa ya Mwenge anawafafanulia wanyama kuwa huo ulikuwa uvumi tu na mawazo yaliyopotosha. Anaeleza kuwa, daktari wa wanyama alikuwa amelinunua gari lile kutoka kwa mchinjaji lakini akasahau kuyafuta maandishi na jina baada ya kulinunua. Katika mataifa mengi yanayojiendeleza viongozi hutumia ulaghai kuwadhibiti wananchi na kuwaposha kwa kila hali. Aidha, hubadili misimamo yao ya kisiasa na kukarabati kaulimbiu zao, maono na sera ili kujilinda bila kuwajali wananchi waliowachagua.

## 5.0 Hitimisho

Riwaya ya *Shamba la Wanyama* inaangaza mapinduzi kutoka ubepari hadi usoshalisti kwa kutumia wahusika wanyama. Mapinduzi yenyewe ni zao la ndoto ya nguruwe mzee anayeitwa Mbalamwezi. Kwa kutumia anthropomofiki, mwandishi anadhihirisha mfululizo wa mapinduzi kupitia elimu. Lengo kuu la makala haya liliafikiwa na watafiti baada ya mjadala ulioongozwa na mihimili miwili mikuu ya Nadharia ya Uhakikimazingira kujadiliwa. Tathmini ya matumizi ya anthropomofiki na mtunzi Orwell imedhihirisha kuwa itafika siku wananchi katika mataifa mengi, hasa fukara ya Afrika watachukua mamlaka mikononi mwao na kuudidimiza ukoloni mamboleo. Kupitia anthropomofiki Orwell anaikosoa jamii na kuielimisha kuhusu haja ya elimu katika mapinduzi. Orwell anawatumia nguruwe kuwasawiri viongozi binafsi, walaghai na wenye tamaa wa Afrika. Viongozi hawa hujali nafsi zao pekee na namna wanavyoweza endelea kuwanyanyasa watu na kuwatumia kwa manufaa yao.

**Marejeleo**

Airenti, G. (2018) "The Development of Anthropomorphisim in Interaction: Intersubjectivity, Imagination, and Theory of Mind". *Frontiers in Psychology*. Juz. 9 (1): 1-13. Inapatikana katika https://doi.org/10.3389/fpsyg.2018.02136. Ilisomwa tarehe 7 Aprili 2021.

Alia, A. (2017) *Ecocritical Post-Colonial Studies on Humans, Land and Animals*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nothern Iowa, Iowa.

BAKITA (2015) *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Bladow, K. & Ladino, J. (Wah.) (2018) *Affective Ecocriticism: Emotion, Emdodiment, Environment*. USA: University of Nebraska Press Lincoln and London.

Buell, L. (1996) *The Environmental Imagination: Thoreau, Nature Writing, and the Formation of American Culture*. Cambridge: Havard University Press.

Dacey, M. (2017) "Anthropomorphism as cognitive bias." *Philossophy of Science Association*. Juz. 84(5): 1152-1164. Inapatikana katika https://doi.org/10.1086/694039. Ilisomwa tarehe 10 Aprili 2021.

Filipova, L. (2023) *Ecocriticism and the Sense of Place* (Toleo la 1). New Delhi: Routledge.

Garrard, G. (2007) "Ecocriticism and Education for Sustainability". *In Pedalogy: Critical Approaches to Teaching Literature, Language, Composition & Culture: Duke University Press*. Juz. Na. 7(3): 359 -386.

Garrard, G. (2023) *Ecocriticism* (Toleo la 3). Philadephia: Routledge.

Glotfelty, C. & Fromm, H. (Wah.). (1996) *Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology*. Athens and London: The University of Georgia Press.

Iheka, C. N. (2015) *African Literature and the Environment: A Study in Postcolonial Ecocriticism*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Michigan State, Michigan.

Larsen, N. E., Lee, K., na Ganea, P. A. (2018) "Do Storybooks with Anthropomorphized Animal Characters Promote Prosocial Behaviors in Young Children?" *Developmental Science*.Juz. 21(3): e12590. Inapatikana katika https://doi.org/10.1111/desc.12590. Ilisomwa tarehe 15 Aprili 2021.

Leech, G. (2013) *Language in Literature: Style and Foregrounding (Toleo la 1)*. London: Routledge.

Maathai, W. (2009) *The Challenge for Africa*. Britain: William Heineman.

Marx, K. (1867) *Das Kapital* (Toleo la 1). Verlag von Otto Meisner.

Mdee, J. S., Njogu, K. na Shafi, A. (2015) *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Megan, S. G., Gretchen, A. W. na Vanessa, L. (2015) "Learning About Real Animals From Anthropomorphic Media." *Imagination, Cognition and Personality: Consciousness in Theory, Research, and Clinial Practice, SAGE*. Juz. 36(1): 1 – 22. Inapatikana katika https://doi.org/10.1177/0276236615611798. Ilisomwa tarehe 20 Aprili 2021.

Morris, P., Lesley, S., na Knight, S. (2012) “Belief in Animal Mind: Does Familiarity With Animals Influence Beliefs About Animal Emotions?” *Society & Animals*. Juz. 20(3):211-224. Inapatikana katika https://doi.org/10.1163/15685306-12341234. Ilisomwa tarehe 23 Aprili 2021.

Muhia, A. K., Mwamzandi, I. na Kisurulia S. (2019) “Utandawazi na Elimu Tumizi Barani Afrika: Haja ya Mustakabali Mpya kwa Mujibu wa *Dunia Yao, Msimu wa Vipepeo na Nakuruto*.” *East African Journal of Swahili Studies*. Juz. 4(1): 68-79.

Mulokozi, M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Muriithi, J. J. (2017) *Itikadi Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Njeru, M. K., Kobia, J. M. & Musyimi, D. M. (2022) “Motifu ya Ukame katika Tamthilia za *Janga la Werevu* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015).” *East African Journal of Swahili Studies*.Juz. 5(1), 183-195. Inapatikana katika https://doi.org/10.37284/eajes.5.1.733. Ilisomwa tarehe 28 Aprili 2021.

Oliver, L. (2016) *The Postcolonial Intellectual: Ngugi wa Thiong’o in Context*. New York, NY: Routledge.

Onyango, J. O. (2011) “Imagery as a Pervasive Feature of Style: The Case of Ebrahim Hussein’s *Mashetani* (1997).” Katika J.K. S. Makokha, E. Kabaji & D. Dipio (Wah.). *East African Literature: Essays on Written and Oral Traditions*: Logos Verlag Berlin. Kur. 399 – 414.

Orwell, G. (1945) *Shamba la Wanyama*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Peterson, C. (2022) “The Plasticity of Race: Microaggressions and derridean Postracism.” *Journal of the Theoretical Humanities*. Juz. 27(5): 162-173. Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/09697225x.2022.2110402. Ilisomwa tarehe 18 Februari 2021.

Slovic, S., Rangarajan, S. & Sarveswaran, V. (Wah.) (2020) *Routledge Handbook of Ecocriticism and Environmental Communication* (Toleo la 1). Routledge.

Tan, C. (2019) *An Ecocritical Study of J. G. Ballard’s Climate Fiction Novels*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Pamukkale, Pamukkale.

Thiong’o, N. (1987) *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature.* Harare: Zimbabwe Publishing House (Pvt.) Ltd.

TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 4). Nairobi: Oxford University Press.

Waithiru, A. K. (2019) *Matumizi ya Taashira Kuangaza Jiografia na Utandawazi Katika Tamthilia za Zilizala na Sudana*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia, Nyahururu.

Waithiru, A. K., Nabea, W. K., na Onyango, J. O. (2021) “Uamilifu wa Taashira Katika Tamthilia za *Zilizala* na *Sudana*.” *Mwanga wa Lugha Jarida la*

*Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Chuo Kikuu cha Moi*. Juz. 6 (1): 43-54.

Waithiru, A. K. (2022a) "Symbols of the Sentient House of Usher: An Ecocritic Approach." *East African Journal of Education Studies*. Juz. 5(2): 369-376. Inapatikana katika https://doi.org/10.37284/eajes.5.2.812. Ilisomwa tarehe 7 Februari 2023.

Waithiru, A. K. (2022b) "An Evaluation of Environmental Symbolism used in Children Literature: Case Study of *Kijiji Cha Ukame* and *Mazingira Maridadi." East AfricanJournal of Education Studies*. Juz. 5(3): 1-10. Inapatikana katika https://doi.org/10.37284/eajes.5.3.846. Ilisomwa tarehe 14 Februari 2023.

Waithiru, A. K. (2022c) "Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya *Sudana*." *East African Journal of Swahili Studies*. Juz. 5(2): 124-130. Inapatikana katika https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010. Ilisomwa tarehe 20 Januari 2023.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.